



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA
BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA



TANGAZO KWA WAENDESHA GHALA WOTE

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi chini ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa Sheria Namba 10 ya Mwaka 2005 na marekebisho yake chini ya Sheria Namba 4 Sura ya 339 R.E. 2016. Bodi imepewa majukumu chini ya Kifungu 5 (a-j) cha Sheria hiyo ikiwemo kutoa leseni kwa Waendesha Ghala, Meneja Dhamana na Wakaguzi wa Ghala.

Bodi inapenda kuwajulisha waombaji leseni na wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwa imeandaa mafunzo ya wafanyakazi wa ghala kuanzia tarehe **24 hadi 26 Septemba 2022** katika **Ukumbi wa Chuo cha Kilimo Mtwara (MATI)** mkoani Mtwara.

Mafunzo haya yanalenga wafanyakazi watano kisheria ghalani ambao hawakuwahi kupita mafunzo na mitihani inayotolewa na Bodi. Aidha, wadau wengine wenye nia ya kujifunza shughuli za usimamizi wa ghala kama vile wakurugenzi wa kampuni za waendesha ghala, wanunuzi na wengineo wanakaribishwa. Mafunzo haya yatahitimishwa kwa mtihani pamoja na vyeti kwa watakaofaulu.

Mafunzo haya yatafanyika kwa siku tatu. Gharama ya mafunzo kwa mhusika ni **shilingi 750,000**.

Aidha, katika siku ya kuhitimisha mafunzo ya **tarehe 26 Septemba 2022** wakurugenzi na mameneja wote wa kampuni zinazotarajia kuendesha ghala msimu wa korosho 2022/2023 wanapaswa kuhudhuria kikao cha maandalizi ya msimu na kuhitimisha mafunzo kitachofanyika **kuanzia saa sita kamili** mchana katika ukumbi huo.

Kwa mawasiliano ya kuwasilisha majina yawatakahudhuria mafunzo na maandalizi ya vyeti utawasiliana na **Afisa Rasilimali Watu-WRRB 0767 619 469**. Kwa mawasiliano kuhusu malipo na kuandaliwa *control number* utawasiliana na **Mhasibu-WRRB 0713 724 933**;

Imetolewa,

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji

05 Septemba 2022